**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU –TAMISEMI**

**Namba za Simu.**

**Mkuu wa Shule: 0786631524**

**Makamu Mkuu wa Shule: 07667291378/0625893213**

**Matron: 0656-608992 / Patron: 0620-772193.**

**Shule ya Sekondari UYUMBU,**

**S.L.P 151, URAMBO.**

**Tarehe………………..**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**.S.L.P**

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI UYUMBU HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO MKOA TABORA MWAKA………………….**

1. Uongozi wa shule ya sekondari Uyumbu unafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano katika Shule hii mwaka ……………..na atasoma tahasusi ya .
Shule ya sekondari Uyumbu ipo mkoa wa Tabora wilaya ya Urambo tarafa ya Ussoke Kata ya Uyumbu. Shule hii ipo umbali wa km 19 kutoka Ussoke na km 50 kutoka Urambo. Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi **URAMBO /TABORA** Nauli ni Tzs.5000/= (elfu tano tu) kutoka Urambo na Tzs. 6000/= (elfu sita tu)kutoka Tabora hadi shuleni au akichelewa mabasi atashukia Ussoke kisha atatumia usafiri wa pikipiki kwa nauli ya Shilingi Tzs.8,000/= (Elfu nane tu) hadi shuleni. Shule yetu ni ya mchanganyiko na shule ina wanafunzi wa kidato cha kwanza mpaka cha sita. Kidato cha tano hadi cha sita kuna tahasusi za **HKL**, **HGL**, **HGE**, **PCB na PCM.**
Muhula wa Masomo unaanza tarehe………………….hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe………………..Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………………………….

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

**WASICHANA**

i. Sketi (2) linda box ya malinda rangi ya kijivu iliyokolea (dark grey) ndefu zivuke magoti kwenda chini mpaka kifundo cha mguu na kitambaa kiwe kizito.
ii. Mashati meupe mawili (2) mikono mirefu.
iii. Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba kisigino kifupi.
iv. Soksi ndefu nyeupe.
v. T-shirt 2 rangi ya njano zenye kola na vishikizo kifuani.
vi. Tai ya rangi ya Kijivu iliyokolea (dark grey).
vii. Hijab/Juba jeupe la darasani kitambaa cha Halwa na Juba la kushindia rangi ya njano. Hijab/juba zote ziambatane na nusu kanzu ya kitambaa husika.
viii. Sketi nyeusi mbili za marinda za kushindi ndefuzivuke magoti kwenda chini mpaka kifundo cha mguu na kitambaa kiwe kizito
ix. Sweta rangi ya kijivu.
x. Hijabu ya kushindia rangi ya njanokwa waislam

NB. **Vipodozi na pafyumu za aina yoyote, wanja, piko, rangi za midomo/kuchaHAVIRUHUSIWI.**

**WANAFUNZI WA KIKE HAWARUHUSIWI KUSUKA NYWELE.**

**WAVULANA**

i. Suruali (2) ndefu hadi kwenye kisigino cha mguu zenye marinda rangi ya kijivu iliyokolea (Dark grey)SIO **MODO** na kitambaa kiwe kizito chini size 17.
ii. Mashati meupe (2) mikono mirefu,
iii. Sweta rangi ya kijivu,
iv. T-shirt 2 rangi ya njano zenye kola zisizo na maandishi
v. Viatu vyeusi vya Kamba visigino vifupi na soksi nyeusi,
vi. Suruari nyeusi ndefu mbili (2) za kushindia zenye marinda na kitamba kiwe kizito
vii. Tai rangi ya kijivu (Dark grey). viii.
Mkanda wa ngozi mweusi

**VIFAA VYA MICHEZO.**

i. Bukta na t-shirt rangi ya blue (T-shirt isiwe na maandishi) jezi za vilabu vya mpira haziruhusiwi (wavulana).

ii. Track suit na t-shirt rangi ya blue (zisiwe na maandishi)/ jezi za vilabu vya mpira haziruhusiwi - (wasichana).
iii. Raba jozi moja.

**2.2Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari counter book Qa au Qz angalau daftari 10 na kalamu za kutosha. ii. **Ream (A4)mbili** (2) ya Karatasi kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

v. Scientific Calculator fx 991 kwa tahasusi ya PCM na PCB

vi. Godoro futi $2\frac{1}{2}$ x 6

vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya blue bahari, foronya ya godoro 1, chandarua viii. Nguo za ndani za kutosha;

ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

xi. Kwanja 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje kwa wanafunzi wote xii. Jembe lenye mpini kwa tahasusi ya PCM, PCB, HGL na HGE

xiii. Panga kwa tahasusi ya HKL

xiv. Sanduku la chuma kwa ajili ya kuhifadhi vitu vyake na kufuli.

xv. Sabuni, mafuta ya kupaka (Baby soft, vaselline, vaselline jelly, nivea jelly, samona, moviet), dawa ya meno na mswaki vya kutosha.

**2.3Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla kuu** | **80,000/=** |

Lipia benki ya NMB kwa akaunti namba 51301100031 UYUMBU SEC. REV. COLLECTION ACCOUNT. **Hakikisha unapolipa andika jina la mwanafunzi na unawasilisha pay in slip wakati wa kuripoti shuleni.**

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Kutotii wito wa kengele yoyote inayokutaka kuwepo eneo husika (mfano Pared n.k). Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na kuvuta sigara
ix. Uasherati, kusagana, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba na kusabisha mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi pamoja na kifaa chochote kinachotumia umeme (electronic devices) katika mazingira ya shule na nje ya eneo la shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kuwa nje ya eneo la shule bila kuwa na kibali maalum
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xviii. Kutohudhuria vipindi vya darasani na muda wa maandalizi wa jioni, usiku na alfajiri (preparations)
xix. Kukutwa bweni wakati wa vipindi vya darasani na muda wa maandalizi ya jioni usiku na alfajiri (preparations)
xx. Kukutwa kwenye vichochoro au maeneo ya giza ukiwa peke yako, kundi wa wanafunzi au jinsia mbili tofauti.

**NB:HAKIKISHA ENEO ULIPO WAKATI WA USIKU KUNA MWANGA WA KUTOSHA, KAMWE USIKAE/KUSIMAMA ENEO LENYE GIZA.**

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Jina 1a Mkuu wa shule

Mhuri wa Mkuu wa Shule

**NB**: **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au** Kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA **KWA NAMBA** ZIFUATAZO:

Mkuu wa shule 0786631524
Makamu Mkuu wa Shule 07667291378/0625893213
Mwandamizi Taaluma 0656-608992
Malezi na nidhamu 0620-772193/0765-805986

**HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO**

**SHULE YA SEKONDARI UYUMBU.**

**KIAMBATISHO (A)**

Nenda na fomu hii kwa mganga wa serikali akakupime na kukujazia

..................................

..................................

........................

..................................

Tarehe........................

..................................

Mganga,

S.L.P

.........................................................................................

MEDICAL CERTIFICATE:

Jina ................................................ la

mwanafunzi..................................................................................

..................................

.........................................................................................................

1. Nimempima mtajwa hapo juu na kumuona amepatikana na ugonjwa wa na nimemtibu ipasavyo.

2.Nimempima mtajwa hapo juu na kumuona na ugonjwa hawezi kusoma kwasababu ya

..................................................................................

..................................................................................

..................................................................................

..................................................................................

..................................................................................

3. Kwa wasichana tu, nimemwona ana mimba/ hana mimba.Tutakayemtilia mashaka tutampeleka hospitali kwa daktari wa hapa wilaya ya Urambo.

4. Afya yake kwa ujumla.

a) Kifua
b) Macho
c) Masikio
d) Kilema chochote kitaje
e) Akili
f) Mkojo (urine)
g) Choo (stool)
h) Mimba

Sahihi ya mganga

Mhuri:

Tarehe

**HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO**

**SHULE YA SEKONDARI UYUMBU,**

**S.L. P 151, URAMBO.**

## HISTORIA YA MWANAFUNZI: FOMU (B)

1. Jina la Mwanafunzi: .
2. Tarehe kamili ya kuzaliwa: .
3. Jina la Baba: .
4. Jina la Mama: .
5. Jina la Mlezi: .
6. Anuani kamili ya Mzazi/Mlezi: .
7. Uhusiano wa Mlezi: .
8. Kazi ya Mzazi/Mlezi (Mkulima, Mfanyakazi,Mfanyabiashara) .
9. Kama ni Mfanyakazi, kazi yake: .
10. Kama Mkulima zao muhimu analotegemea: .
11. Kama Mfanyabiashara, Biashara yake: .
12. Afya yake (Maelezo kama mwanafunzi anayomatatizo ya kiafya na hivyo anastahili huduma maalum) .
13. Madhehebu ya dini ya Mwanafunzi: .
14. Jamaa, Ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya Mzazi/Mlezi;

| NA | JINA KAMILI NA ANUANI YAKE | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

15. Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi:
    Mimi: Nathibitisha kuwa maelezo yaliyotajwa hapo juu ni sahihi.
    Anuani ya Mzazi/Mlezi: Tarehe: .

**HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO**

**SHULE YA SEKONDARI**

**UYUMBU, S.L.P 151,**

**URAMBO.**

## KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE: FOMU (C)

1. Jina la mwanafunzi:……………………….…………………………………….
2. Jina la mzazi/mlezi:…………………………………………………………….

Mimi…………………………………………………………………………………
nimechaguliwa kuwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Uyumbu, nakubali nafasi hii niliyopewa na serikali ya Tanzania. Naamini kabisa nimetunukiwa nafasi hiyo iii niliendeleze kwa manufaa ya watanzania. Hivyo ninaahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa shuleni, nje na ndani ya darasa. Iii kutimiza shabaha hii ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa BUSARA, MAARIFA, NIDHAMU YA HALI YA JUU na UTII kwa viongozi wote kwa sheria na amri za shule. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi Tarehe .

Mimi................................................... nikiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi naahidi kuwa
nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyu na kushirikiana na shule na nitakuwa tayari kulipa gharama za uharibifu wowote utakaojitokeza wa mali za Umma/Shule utakaokuwa umefanywa na mtoto wangu.

Sahihi ya mzazi/mlezi. Tarehe .




SARE YA SHULE



SARE YA NJE YA DARASA



**SARE YA MICHEZO KWA WOTE**